

MTU WA ASILI NA MTU WA KIROHO

1 wakorintho 2:6-16 “.....maana ni nani katika binadamu ajuaye mambo ya binadamu ila Roho ya binadamu ya ndani yake?. Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu.lakini sisi hatuku pokea Roho ya dunia bali Roho atokeya kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena si kwa maneno tunayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu bali tunayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya Rohoni kwa maneno ya Rohoni. Basi

Mwanadamu wa tabia ya asili haya pokea mambo ya Roho ya Mungu: maana kwake huyo Ni upuuzi, wala hawezi kuyafahamu kwa kuwa yatambuliana kwa jinsi ya Roho. Lakini mtu wa Rohoni huyatambua yote yala yeye hatambuliwi na mtu. Maana ni nani aliyeifahamu nia ya bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo niaya kristo.

Ni dhahiri sana kotokana na haya maandiko kwamba hakuna mtu ambaye yeye mwenyewe anaweza kumsikia Mungu. (**Mathayo 16:17**). “na Yesu akijibu na kumwambia. Umebarikiwa wewe, Simon Baryona: kwa kuwa linadamu havikukufunuliwa wewe, bali / lakini baba yangu aliye mbinguni. Weka pamoja hii mistari tunaona kwamba kuna kundi moja tu la watu, na hilo ni kundi maalum la watu ambao wanaweza kusikia kile Roho amesema katika kila kizazi. Na kundi moja maalum ambalo hupokea ufunuo kwa kila kipindi. Hilo kundi ni la Mungu, kwasababu kundi ambalo haliwezi kusikia siyo la Mungu. (**Yohana 8:42-44**). Kundi ambalo linaweza na linasikia kila Roho anasema nakupokea ufunuo hilo ndilo linaelezewa katika (**1 Wakoritho 2:6-16**). Wao wale ambao wamezaliwa na Mungu wao wamebatizwa ndani ya ule mwili wa Bwana Yesu kristo kwa Roho wake Mtakatifu. [1]

Mtu wa asili, kwa maarifa, anaangalia nyuma kwaajili ya mafanikio yake, hiyo ni sayansi wanatazama kila alichokifanya Mungu katika uumbaji wa zamani. Wao wanatoka nje na kuchukua mabonge na vipande vya miamba na mabaki na viumbifu element na kuvifunga manisha hivyo pamoja. Na unaona, katika hayo mafanikio, wanachukua kile Mungu alichofanya na kupotosha hilo kutoka katika mahali pake pa asili na kutengeneza au kufanya Roho yake ya kuishi na kadhalika na uchumi wake ni bora zaidi, kwa kile kilichoumbwa. Na hayo ni katika mafanikio ya asili kwa mwanadamu. Lakini Mungu, katika mafanikio ya kristo, unaendelea mbele, sio kuludi nyuma. Yeye anaendelea mbele , akiangalia katika neno na akiamini ahadi kwa mabo ambayo kamwe hajakuja bado, kwa ufunuo wa

ki Roho kuweka wazi mambo mambo ya kiroho ambayo Mungu ameahidi. Yeye anawaona wao wakijapita. Kama tu mwanasayansi katika maabara anafanya kazi katika mambo tofauti kumsaidia mtu/ mwanadamu, akichukua uumbaji mtu wa kiroho angalia mbelle kile ambacho Mungu ameahidi. Ambacho hakijawahi kuumbwa (**2Wakorintho 3:18**). Mtu wa asili hutazama nyuma. Mtu wao kiroho hutazama mbele. Hiyo ndiyo njia wanazo katika kanisa. Wanachama wakanisa la asili wanaangalia nyuma kwa Finney, Sankey, Knox caloin hiyo ilikuwa ni sawa, lakini hiyo ilikuwa siku yao. Tunaangalia mbele Kwa kitu Fulani, ahadi ilyo kuu na juu. Mno na kila Mungu ameahidi. Sayansi inarudi nyuma, Ili kuipata. Tunaendelea mbele, katika neno la Bwana, kupata kila Mungu alifanikiwa.

Angalia, mtu wa asili pia anahesabu kinyume nyumbe. Nilisema yeye hufanya mambo kinyume nyumba, yeye huhesabu kurudi nyuma. Angalia kuhesabu kwake , “kumi, tisa, nane, saba, sita , tano, nne,tatu, mbili,moja, sifuri!, unaona, yeye aenda nyumbani (katika kuhesabu kinyume nyume) na huanza kuhesbu. [2]

Miili yetu huongezwa Kwa hisi tano. Ni ngapi wanajua hiyo ni kweli? Hisi tano: kuona, kuonya, kuhisi, kunusa, na kusikia, hiyo inamuongoza mtu wa asili. Sasa tu mwingine ndani ambaye ni mtu wa Imani, Roho (2wakorintho 4:13). Yeye anahisi mbili: moja wapo ni Imani na nyingine ni kutokuamini. [3]

Na nilikua tu nikifikiri muda mchache uliopita juu ya somo la sayansi .Na nilifikiri tu juu ya hiyo sayansi, jinsi wanavyomchukuwa mtu wa asili na jinsi yeye alivyoingia katika utafiti kutoka kuanguka kwa asili na kila yeye alichofanya. Na jinsi mtu mdogo wa kiroho ameendelea katika ufalme wa Mungu. Na nilifikiri kwamba, mtu wa asili alikwenda nje katika kutoona kwa macho yake na kuvuta atom chini kutoka kwenye mbingu / anga,na kugawanywa hiyo atom katika sehemu mbili ambayo huharibu maisha ya binadamu. Na kama mtu wa asili ambaye hajui chochote cha Mungu na hawezi kujua chochote cha Mungu isipo kuwa yeye amebadilishwa, basi nafsi yake inakuwa haina isiyo ya kawaidakama yeye angeweza kufanya hilo katika ulimwengu wa asili, nini mtu wa Mungu angepasa kufanya? Jamani , jamani , marafiki, kanisa liko nyuma sana . hebu tuombe kwamba Mungu atalisogeza kanisa lake ju. Mtu wa asili/ wa kawaida pamoja na raslimaliza asili wanapata matokeo makubwa kuliko watu ambao wanajiita wenyewe wakristo. Hebu tuingie ndani ya wasioonekana! (**Luka 16:16:2 Wafalme 6:14-17**). Baraka ni zenu, ziko kwaajili yenu! [4]

Mtu asili anahisi tano tu. Lakini mwaminio, wakati anapokutana na Mungu, yeye anapata kitu Fulani cha tofauti, hiyo ni hisi kuu ambayo humwinua juu kupitia vivuli. Inamfanya yeye aamini vitu ambavyo havionekani kuja kutokea

(Waefeso 3:20-21) Yeye huendelea kuamini yatakuja kutokea, kwasababu Mungu amesema hivyo. Wakati mtu anapokutana na Mungu, kitu fulani hutokea **(2Wakorintho 5:17)**. [5]

Mtu wa kiroho kule ndani, kama utampa yeye usahihi wa njia, yeye atakuongoza kwenye ujumbe mdogo mahali fulani, ambako hakuna watu wengi, lakini kuna Roho wa Mungu aishiye. Kwa mtu wa nje anakula katika saikologia na mambo ya kiakili. Lakini mtu wa ndani anakula katika neno la Mungu **(Mathayo 4:4)**. [6]

Mimi ninajaribu kulileta kwao, Bwana, kwamba mtu wa kawaida huona vitu vya kawaida. Na hapo, na mambo ya kiroho yako kinyume na akili, hivyo yeye hawezi kuelewa hilo. Na ulikuwa ni wewe, Bwana, uliemwambia Nikodemo, “Isipokuwa mtu awe amezaliwa mara ya pili, yeye hawezi hata kuelewa Ufalme wa Mungu” **(Yohana 3:3-5)** [7]

Kwanini Haruni alikua kifuni mwake na mawe ya uzao kwa kila moja ya makabila? **(Kutoka 28:15-30); (Hesabu 27:18-21); 1Samweli 28:6; Walawi 8:1-13)**

Anglia mama wale wakati wakitoa maneno yao. Wakati mama zao na wanawake wa kiebrania wanapofanya kazi wanawaambia watoto zao ambao wamezaliwa, iliweka majina yao, iliwaambia kuzaliwa kwao, ili waweke wao katika nchi ya nyumbani na kuwaweka kwa umilele. Hiyo ni sawa. Na halafu muangalie Yakobo, wakati anakufa pale, wakati anaweka mikono yake juu ya wale wazee wa makabila na kuwabariki, aliwaambia wao hasa ambapo wangukuwa. Na hiyo ni sawa kulingana na majina yao, na ni sawa kulingana na uzazi/uzao wao. Na hakika, lina kitu Fulani la kufanya na wewe. Sasa, hiyo njia yako ya kuzaliwa; hivyo ndivyo ulivyo mwanamume wa kawaida au mwanamke wa kawaida. Lakini wakati wewe umezaliwa mara ya pili, hiyo siyo dhamiri ya nje. Nje ni kile unachokiona, kuonja, kuhisi, kunusa, na kusia, lakini ndani ya hayo ni kile wewe ulichohalisi. Sasa, hii hapa, shetani hukujaribu tu wewe na kukugonga wewe kila njia hapa; lakini chini hapa yeye hawezi kufanya hilo mpaka umuache yeye kufanya hilo. Kwa maana ndani hapa unaamini, na Imani haiji kutoka dhamiri ya nje, hiyo ni sababu. Lakini ndani ya Imani hakuna hoja unapata hiyo kutoka kwa Mungu, na unajua iko pale **(Marko 11:22)** sijali inaonekana ya makosa kiasi gani, bado unajua ni sawa. Ni hii asema Bwana. Unaona? Na hakuna chochote kitaenda kudhuru hilo. Hakuna kinachoweza kudhuru hilo. Lina songa moja kwa moja likiendelea. Kigumu hakimaanisha chochote kwa hilo. Hupoteza haki kupitia

hilo, kwa maana ni neno. Na neno ni upanga (**Waefeso 6:17**) na neno hukata. Upanga hukata lenyewe kutoka katika kila kitu. Unaona. Huchukua mkono wa imani kushikilia hilo neno. [8]

Je wana na binti wote wa waaminini wa kweli waliozaliwa mara ya pili, wataokolewa? Hapana, ndugu hapana, wao hakika hawataokolewa. Unaona, kama nilivyomnukuu Davidi du plessis juu ya msemu huu “ Mungu hana wajukuu, kama baba zao na mama zao walizaliwa kwa roho (**Yohana 3:5**) unaona? Hiyo ndiyo inayomfanya mtu kuwa mtu mpya ni kwa sababu anazaliwa tena, kuzaliwa upya. Kuzaliwa kwake kwa kwanza kunamfanya kuwa mtu wa asili katika dunia, kuzaliwa kwake kwa pili kunamfanya yeye mtu wa kiroho mbinguni. Unaona? Humbadilisha yeye, nafsi yake, siyo dhamira yake ya nje, nje kwake kunakuwa, hisia zake, yeye anaendelea kuhisi na kunusa, kuonja na kusikia. Lakini sehemu ya ndani matamania yake nini kimemuamasisha yeye, amebadilishwa kwa Mungu (**Waebrania 10:2**) sasa kumbuka njia pekee ambayo hili linaweza kutukia ingekua hii, kama ilivyokua wakati wa Ofisa wa kirumi (**Matendo 16:16-34**). Paulo alimwambia Warumi, yeye na sila, wakati yeye alipotaka kuvuta upanga wake na kujiua mwenyewe, kwa sababu Mungu alitupa jela chini kwa tetemeko la ardhi. Yeye akasema, “usijidhuru wewe mwenyewe, angalia huko hapa wote. Simama” na alihitajika kujua kile yeye angefanya. Yeye alisema, inuka na ubatizwe aliitaye jina la bwana na wewe na nyumba yako yote mtaokolewa. Unaona? Kwa maneno mengine, muamini Bwana yesu Kristo, uleule na nyumba yako mtaokolewa. [9]

Tumefundishwa kwamba Mungu amempa mtu wa kawaida hisi tano kuwasiliana na mazingira yake ya duniani, na hizi zote zinajulikana kama. Kuona , kuonya, kuhisi, kunusa kusikia hisi zote hizo tano ambvazo zinzjulikana kwa mtu kawaida. Na hizo ni nzuri hatuwezi kuishi maisha ya kawaida wakati mmoja kati ya hizi hisi inaposhindwa kutenda kazi kuona kwako, kusikia ,kuhisi, kunusa au kuonja , hatuwezi kuwa sawa bila hizo. Kuna kitu fulani kimepunguka, sehemu fulani ya maisha ambayo hatuwezi kuwasiliana nayo bila hiyo hisi kutenda kazi. Na hizo ni nzuri na zinatumiwa, na tumepewa hizo na Mungu. Mungu ametupa hizo hisi, lakini hivyo vimepewa kwako kama kipawa. Na inategemea kwamba unazifanyia kazi kwa jambo gani ndivyo maisha yako yatakavyoongozwa vile unavyo ruhusu zile hisi tano.....yale unayoona, yale unayosikia, kile unachoonja ama kugusa au kunusa, vitu vyote vinavyo ruhuswa na hizo hisi vitakutawala. [10]

Sasa na marudio yetu milele hayatambuliwi kwa yale tunayo yaoona na kwa yale tunayoyasikia, lakini unatambuliwa kwa ule utambuzi tulionaokwa kile tunachoona na kile tunachokisikia. [11]

Na tunamshukuru Mungu kwamba tunazo hisi tano, bali kwa vyovyote vile hakupewa hizi hisi tano zipate kukuongoza Wewe. Zilitolewa kwako Kwa ajili ya mawasiliano ya duniani. Lakini amepewa wewe hisi ya sita na hisi ya sita ni mkirsto tu na hawezi kuwa na hiyo hisi ya sita mpaka wewe umekua mkisto, ndiyo njia pekee ambayo unaweza kuwa na zaidi ya hisi hizo tano za kawaida kwa mtu wa kawida. Lakini hisi ya sita inajulikana vizuri zaidi kwa mkristokama Imani (**2Wakorintho 4:13**).hiyo ndiyo inayokutawa na kukuongeza na ni ya hali ya juu kuliko hizo hisi zingine zote. Ni ya hali ya juu kuliko hisi zote, hizo hisi zingine tano, sas, nisingeweza kusema kwamba kwasababu tumepokea ile hisi ya sita kwamba zile hisi tano hazifai tena. Ndiyo zinafaa. Hisi tano ulipewa na Mungu nazo zinapaswa kutumiwa na lakini zile hisi tano zinazotenda kinyume na neno la Mungu, basi zinadanganya. Ni hisi kuu. Na hisi kuu ni Roho mtakatifu, Imani ya Mungu ambayo inakaa ndani yako (**Wagalatia 2:19-20**) na utaacha zile hisi tano kutii hisi ya sita, itakuongoza wewe na kuleta zile hisi zote tano chini ya uongozi wa ile hisi kuu kwa kua iko Juu sana zaidi ya hisi ya kawaida kama vile mtu wa kiroho alivyo juu ya mtu wa kawaida iko juu sana kama mbingu zilivyo juu sana, juu zaidi ya mtu wa kawaida na hisi zote tano. Inakufanya wewe uamini mambo ambayo huwezi kuyaona. Inakufanya utende ambavyo ufikiri zile hisi tano zilivyopata kuanzia la husu hilo. Shetani anaweza kuingia katika hizi hisi tano za kukudanganya wewe. Lakini hawezi kugusa hiyo hisi kuu. Iko mbali sana na anapoweza kufikia. Inatoka kwa Mungu. Inaitwa Imani ndicho hicho kitu kikuu [12]

Mtu hawezi kuelewa kwanini watu wanapiga makelele. Mtu hawezi kuelewa kwanini mwanadamu lugha anaweza kubadilika na yeye hawezi kuonana kwa lugha. Mtu wa kawida hawezi kuona jinsi utukufu wa Mungu weza kuja kwenye macho ya mtu nayeye angeweza kuona maono na kumwambia mtu baadhi ya mambo na nini cha kufanya: na kuwaambia wao mambo ya kurekebisha ambayo yameshatokea na kurekebisha mambo ambayo ya ngekuja. Akili ya kawaida hujaribu kulitathmini hilo. “vema ni nini amefanya?au ni aina gani ya utapeli unatumia ?ana akili macho cha maana gani?” kumuona mtu akinena kwa lugha na mtu Fulani akitafsiri na kuuwambia kabisa baadhi ya wanachama kile wao wamefanya na kile wao wasinge paswa kufanya (**1 wakorintho 12:4-11, 14:10-16**)wanafikiri ni aina Fulani ya utapeli. “Kuna kitu Fulani kimefungwa kati yao”.

Hawawezi kulewa hilo mapaka Yule mtu azaliwe mara ya pil. Halafu wakati amezaliwa upya, basi anakua kwenye mstari wa ushirika, kwasababu yeye ni kiyinbe kipya. Zile tuhuma za kale, tabia ya mashaka azilzokua, zinakufa .sasa, yeye ni kiumbe kipya (**2 wakorintho 5:17, wagalatia 6:14-15**).

Angalia, anapaswa kuzaliwa mara ya pili. Na wakati amezaliwa mara ya pili, hawezi kuzaliwa mara ya pili bila kua na Imani. Huyu ni sawa. Imani ni msingi wa yote hayu (**2petro 1:5-11**).

“kwa maana bila Imani hatuwezi kumpendeza Mungu. Yeye amuendeaye Mungu lazima aamini yeye. Yupu na hawapati thawabu wale wamtafutao yeye”

(**Waebrania 11:6**). Dhambi ni nini? Kutokuamini (**Yohana 16:8-11**) kuna vitu viwili tu vinavyo muongoza mwanadamu. Hiyo ni shaka au Imani, kimoja au kingine. Wewe unamilikiwa na yule anayetawala maisha yako. Inategemea ni Imani kiasi gani unayo,unaweza kuinuka kiasi gani. Lakini, kwanza, inapaswa kua Imani. Sasa Imani lazima ni kile unachoamini. “Imani ni bayana ya mambo ya tarajiwayo”. Unacho hicho tayari wakati unaimani, kwasababu linafunuliwa Kwa Imani. “ Imani ni bayana ya mambo yatalajiwayo” Waebrania 11:1, unaona. “ushahidi”. Ni nini? ushahidi wa aina gani? Ushahidi mtakatifu. [14]

Sasa, Imani ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Hapo ndipo ninapo taka kukaa, kwa muda tu. Ni ufunuo. Yeye amelifunua kwako kwa neema yake. Hakuna chochote umefanya. Wewe hukufanya kazi mwenyewe juu ya imani. Wewe kamwe hukuwa na Imani: Imepewa kwako kwa neema ya Mungu (**Mathayo 16:13-19**). Na Mungu amefunua hilo kwako, hivyo basi Imani ni ufunuo. Na kanisa lote la Mungu limejengwa juu ya ufunuo.

Katika kundi la latazamaji la watu, ambapo mstari wa maombi ungepitia, utakuta baadhi Na wote walikua watu wazuri, tutasema. Wapo baadhi ambao wanajaribu sana kuamini hilo. Wanajaribu kufanya kazi wenyewe katika hilo. Baadhi hawawezi tu kufanya hilo kabis. Na wengine, ni kwa neema tu, limepewa kwao. Sasa, kunatofauti. Hiyo inafanya hilo. Ni ufunuo halisi kwasababu Imani ni ufunuo wa Mungu. Ni lazima lifunuliwe kwanza [14]

Imani ni nini? Imani ni kitabu fulani kilichofunuliwa wa kwako, haijakua bado. Lakini unaamini litakua. Imani ni ufunuo wa mapenzi ya Mungu. Kwa hiyo, kwa ufunuo! [15]

Nukuu za kiingereza:

1. “wakati wa kanisa la smirna” CAB uk 139
2. “kuhesabu kinyume nyume” (64-0209) aya 36-38, 79-80
3. “Magonjwa na mateso” (50-0100) aya 49
4. “sikuwa muasi kwa maono ya mbinguni”(49-0718) aya E-7
5. “na tangu wakati huo” (59-1231), aya E-24
6. “kuangalia yasioonekana” (58-1003), aya E-14
7. “siku zote za maisha yetu” (59-0612), aya E -36
8. “maswali na majibu” (64-0830M), COD uk. 1083
9. “maswali na majibu”(64-0823M),COD uk 945
10. “hisi kuu” (59-1227E), aya 52-57
- 11.“ kutambua mwili wa bwana” (59-0812), aya 4
- 12.“ kimo cha mtu mkamilifu”(62-1014m) aya 17-18
- 13.“kazi ni imani iliyodhihilishwa” (65-1026) aya 105-117
- 14.“ wapakwa mafuta wa siku za mwisho” (65-0725m) aya 53

Jiwe la kiroho la kujengea na. 46 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald
friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia
magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

Charles E. Y. Kanju.

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@livel.com

Cellphone: 0784 704299/ 0718230098